

# Hawashikiki?

## Mitazamo na maoni ya Watanzania juu ya rushwa

## 1. Utangulizi

Serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Rais Magufuli imezindua mikakati mipya ya kupambana na rushwa. Mikakati hii ni pamoja na kuanzishwa kwa mahakama mahsusi kwa ajili ya kushughulikia kesi za rushwa. Mkakati mkubwa kabisa umekuwa ni kuchukua hatua za papo kwa hapo kupambana na tuhuma za rushwa na vitendo vingine vya ubadhirifu. Wafanyakazi wa mamlaka ya bandari na mapato walifutwa au kusimamishwa kazi pale ushahidi ulipobainisha kwamba kulikuwa na ukwepaji wa kodi bandarini. Usafirishaji wa mchanga wa madini (makinikia/vumbi) ulisimamishwa baada ya kampuni za uchimbaji madini ikiwemo Acacia kutuhumiwa kuidanganya serikali kuhusu thamani halisi ya madini yaliyokuwa yanasafirishwa nje ya nchi. Mamia ya watumishi wa umma kutoka taasisi mbalimbali za serikali wamefutwa au kusimamishwa kazi chini ya kauli ya "kutumbua majipu." Haya yote yamekuwa yakienda sambamba na jitihada kubwa za serikali za kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma na utendaji mbovu wa kazi za umma.

Mikakati hii ya serikali ya Magufuli imekuwa ikipongezwa na kukosolewa pia. Kuna mashaka ya kwamba rushwa imekuwa ni tatizo sugu na la muda mrefu nchini Tanzania, na lilikuwa ni chanzo cha matatizo mengi miongoni mwa wananchi. Mwaka 2014, nusu ya wananchi walisema hakuna namna ya kupunguza rushwa nchini Tanzania kamwe. Hivyo basi mikakati hii mipya inayotumika kupambana na tuhuma za rushwa zimewashangaza na kuwafurahisha wengi. Lakini, wakosoaji wanadai kuwa mchakato wa kupambana

1 *Sauti za Wananchi,* Je, juhudi za serikali zimesaidia vita dhidi ya rushwa?, 2014

Muhtasari huu umeandikwa na umeandaliwa na Twaweza East Africa.

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
+255 22 266 4301 | info@twaweza.org |
www.twaweza.org/sauti

Sauti za Wananchi

Twaweza ni sisi

na rushwa hauzingatii haki za watuhumiwa, pamoja na kitendo cha kuwawekea kinga viongozi wakuu wa nchi waliopita kuhusishwa na kashfa za rushwa za zamani. Zaidi, serikali inafanya vitu vingine vinavyotishia kuathiri vibaya jitihada za kupambana na rushwa kama vile kuminya uhuru wa vyombo vya habari, mijadala ya umma pamoja na kuiondoa Tanzania kwenye Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi.

Muhtasari huu umebeba takwimu zinazohusu mitazamo na uzoefu wa wananchi kuhusu rushwa na maoni yao juu ya namna ya kushughulikia vizuri tatizo hilo. Mara ngapi wanakutana na vitendo vya rushwa serikalini ama kwenye taasisi nyingine? Je, wanafahamu kwa kiwango gani kuhusu kesi za tuhuma za rushwa zilizotawala vichwa vya habari miaka ya hivi karibuni? Je, wanapimaje utendaji wa serikali katika kushughulikia kesi hizi? Je, wanaona tofauti gani ya kiwango cha rushwa kwa sasa nchini Tanzania, ukilinganisha na miaka michache iliyopita?

Takwimu za muhtasari huu zinatokana na utafiti wa *Sauti za Wananchi* unaoratibiwa na Twaweza. *Sauti za Wananchi* ni utafiti wenye uwakilishi wa kitaifa, unaotumia simu za mikononi. Utafiti huu una uwakilishi wa Tanzania Bara pekee (Zanzibar haihusiki). Taarifa kuhusu mbinu za utafiti huu zinapatikana kupitia www.twaweza.org/sauti. Takwimu za muhtasari huu, zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa 1,705 kutoka awamu ya 21 ya kundi la pili la Sauti za Wananchi, zilizokusanywa kati ya tarehe 27 Julai na tarehe 14 Agosti 2017.

Matokeo muhimu ni:


- Wananchi wanasema rushwa ni kitendo cha kutoa fedha kwa ajili ya kupata msaada fulani.
- Nusu ya wananchi wanasema posho zinazotolewa kwa watumishi wa umma baada ya kuhudhuria vikao ni rushwa. Chini ya mwananchi 1 kati ya 20 anasema wafanyabiashara wanaowachangia wagombea wakati wa uchaguzi ili wapendelewe naserikali ni rushwa.
- Wananchi wanasema rushwa imepungua kwa kiasi kikubwa kwenye sekta zote kuliko ilivyokuwa miaka mitatu iliyopita, lakini wanataja polisi na mahakama kuwa wala rushwa wakubwa.
- Uzoefu wa wananchi kukutana na vitendo vya rushwa katika sekta na taasisi zote imepungua ikilinganishwa na mwaka 2014.
- Wananchi wote wanaunga mkono mapambano dhidi ya rushwa, lakini wanatofautiana kwenye namna ya kuendesha mapambano hayo.
- Wananchi wengi wanasema iwapo ushahidi utapatikana unaomhusisha rais wa zamani na rushwa, asiwekewe kinga yoyote.
- Wananchi wengi hawajawahi kusikia kuhusu matukio makubwa ya tuhuma za rushwa, ikiwemo Acacia/sakata la mchanga wa madini.
- Nusu ya wananchi wote wanasema wanasiasa wala rushwa wanapaswa kufungwa.
- Mwananchi mmoja kati ya watatu anafahamu kuhusu mahakama ya rushwa; wawili kati ya watatu wanasema inafanya kazi kwa ufanisi.

# 2. Mambo nane kuhusu rushwa nchini Tanzania

## Jambo la 1: Wananchi wanaelezea rushwa kuwa kitendo cha kutoa fedha kwa ajili ya kupata msaada

Asilimia 73 ya wananchi wanasema rushwa ni kitendo cha kutoa fedha kwa ajili ya kupata msaada. Asilimia 36 wanataja rushwa kuwa ni utoaji wa vitu vya thamani, na asilimia 3 wanasema ni utoaji wa huduma za ngono ili kupata msaada fulani.

**Kielelezo cha 1: Rushwa ni nini?[2]**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*
Awamu ya 21 (Julai-Agosti 2017)

Kwa maoni yao, asilimia 93 ya wananchi walisema kuwa utoaji wa fedha kwa wapiga kura wakati wa kampeni za uchaguzi ni aina ya rushwa. Asilimia 78 walisema utoaji wa fedha ama vitu vya thamani kwa watumishi wa umma ni rushwa, na asilimia 75 walisema wagombea kutoa zawadi kama vile kofia na tisheti ni rushwa.

Matendo mengine yanayoonekana kuwa ni aina za rushwa kwa wananchi wengi ni pamoja na wabunge kupewa fedha ili kupitisha bajeti ya wizara (asilimia 69), ulipaji wa mishahara kwa watumishi hewa (asilimia 65), na vitendo vya wagonjwa kumpa daktari wa kituo cha afya cha umma fedha au vitu kwa ajili ya kupata huduma (asilimia 51).

Kitendo maarufu cha kuwalipa watumishi wa umma posho kwa ajili ya kuhudhuria mikutano kilichukuliwa na asilimia 51 ya wananchi kama rushwa.


Asilimia 26 ya wananchi walisema utoaji wa zawadi kwa mwalimu baada ya mtoto kufanya vizuri kwenye mitihani kwa ujumla ni rushwa.

Hata hivyo suala moja lilijitokeza; wananchi wachache sana (asilimia 3) waliosema kitendo cha wafanyabiashara kutoa fedha kuwasaidia wanasiasa wakati wa kampeni za uchaguzi na kisha kutarajia msaada kutoka serikalini ni rushwa.

---

2 Jibu zaidi ya moja liliruhusiwa


**Kielelezo cha 2: Tadhadhali nieleze kama vifuatavyo ni vitendo vya rushwa:**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 21 (Julai-Agosti 2017)

Asilimia 37 ya wananchi wanataja watu kutaka upendeleo kama sababu moja kuu ya rushwa, na hii hufuatiwa na kukwepa adhabu (asilimia 30) kama sababu nyingine mojawapo, na kupata huduma sahihi (asilimia 24) kama sababu ya tatu.

**Kielelezo cha 3: Kwa mtazamo wako, nini kinachosababisha vitendo vya rushwa?[3]**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 21 (Julai-Agosti 2017)

3 Jibu zaidi ya moja liliruhusiwa


## Jambo la 2: Wananchi wanaona kwamba rushwa imepungua katika sekta zote, hata hivyo bado Jeshi la Polisi lina hali mbaya.

Asilimia 60 ya wananchi wanasema rushwa "ipo sana" katika Jeshi la polisi, hii ikilinganishwa na taasisi au sekta zingine. Hata hivyo, kiwango hiki ni cha chini ukilinganisha na mwaka 2014, ambapo asilimia 89 ndio waliosema hivyo. Asilimia 56 ya wananchi wanasema rushwa ipo sana mahakamani na kwenye vyombo vya sheria.

Katika kila sekta ambapo *Sauti za Wananchi* ilifuatilia mwenendo wa rushwa, wananchi wanaonekana wakisema rushwa imepungua. Hii ni hususani kwenye vyama vya siasa na chaguzi (imepungua kutoka asilimia 85 waliosema "rushwa ipo kwa kiwango kikubwa" mwaka 2014 hadi asilimia 48 mwaka 2017), sekta ya ardhi (asilimia 65 hadi asilimia 35), Mamlaka ya Kodi (TRA) na huduma nyingine za kodi (asilimia 70 hadi asilimia 26), huduma ya afya (asilimia 62 hadi asilimia 26) na elimu (asilimia 42 hadi asilimia 10).

Kushuka kwa vitendo vya rushwa kunaonekana pia nje ya sekta za umma: mashirika yasiyo ya kiserikali (asilimia 10 hadi asilimia 2) na mashirika ya dini (asilimia 10 hadi asilimia 2) rushwa inaonekana kupungua kuliko ilivyokuwa mwaka 2014.

**Kielelezo cha 4: Tafadhali nieleze kwa mtazamo wako jinsi vitendo vya rushwa vilivyoshamiri au kupungua kwenye sekta na huduma hizi? (% wanaosema "vimeshamiri sana"**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Kundi la 1, Awamu ya 19 (Juni 2014) na Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Kundi la 2, Awamu ya 21 (Julai- Agosti 2017)

** Takwimu za mwaka 2014 hazipo*

Asilimia 39 ya wananchi waliokutana na polisi walisema waliombwa rushwa, na asilimia 30, walitoa rushwa hiyo. Wakati huo huo asilimia 36 ya wanaotafuta ajira waliripoti kuombwa rushwa.

**Kielelezo cha 5: Asilimia ya walioombwa na waliotoa rushwa miongoni mwa waliokuwa wanataka huduma Fulani:**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 21 (Julai-Agosti 2017)

Sambamba na mtazamo wao kuhusu rushwa, uzoefu wa wananchi kuhusu rushwa pia umeshuka tangu mwaka 2014. Kwa polisi, ardhi, huduma ya afya, mashirika yasiyo ya kiserikali, maji na kodi, idadi ya wananchi wanaosema kuwa waliombwa rushwa imepungua katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Isipokuwa kwa wale wanaotafuta kazi, ambapo idadi ya wananchi wanaosema kuwa waliombwa rushwa haijabadilika (asilimia 36 mwaka 2017, ambayo imepanda kutoka asilimia 34 mwaka 2014).

**Kielelezo cha 6: Asilimia ya walioombwa na waliotoa rushwa miongoni mwa waliokuwa wanataka huduma fulani:**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 21 (Julai-Agosti 2017)

## Jambo la 3: Zaidi ya nusu ya wananchi wanafahamu mahali pa kuwasilisha taarifa za rushwa

Asilimia 56 ya wananchi wanafahamu mahali pa kuwasilisha taarifa za vitendo vya rushwa vilivyofanywa na watumishi wa umma. Hii inahusisha asilimia 42 waliotaja Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), asilimia 10 waliotaja polisi, na asilimia 4 waliotaja mamlaka za kijiji na mtaa.

Asilimia 38 ya wananchi walisema hawajui mahali pa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa.

**Kielelezo cha 7: Je, unafahamu mahali pa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa vinavyofanywa na mtumishi wa umma?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 21 (Julai-Agosti 2017)

Uelewa kuhusu mahali pa kutoa taarifa za rushwa umeongezeka. Mwaka 2014 ni asilimia 44 ya wanachi waliofahamu mahali pa kuwasilisha taarifa lakini mwaka huu (2017) ni asilimia 56 wanaofahamu. Asilimia 33 ya wananchi walitaja TAKUKURU mwaka 2014, lakini mwaka huu ni asilimia 42 (haijaoneshwa kwenye vielelezo).

Baadhi ya makundi kwenye jamii yana ufahamu zaidi kuliko mengine kuhusu mahali pa kutoa taarifa za rushwa. Asilimia 67 ya wanaume wanaonekana kuwa na ufahamu zaidi kuliko wanawake (asilimia 45). Wazee, matajiri na wasomi wanaonekana kuwa na ufahamu zaidi kuliko vijana, masikini na wenye kiwango kidogo cha elimu.

**Kielelezo cha 8: Je, unafahamu mahali pa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa vinavyofanywa na mtumishi wa umma?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 21 (Julai-Agosti 2017)

Asilimia 70 ya wananchi wanaifahamu TAKUKURU na asilimia 69 wanasema taasisi hiyo inatekeleza vizuri au vizuri sana majukumu yake ya kupambana na rushwa (haipo kwenye vielelezo).

## Jambo la 4: Wananchi wanataka kupambana na rushwa, lakini hawafahamu jinsi ya kufanya hivyo


Asilimia 81 ya wananchi wanakubaliana na kauli isemayo “ni muhimu kuwa wakali katika kupambana na rushwa hata kama itachelewesha maendeleo,” kuliko ile kauli inayosema “tusiwe wakali na kuiachia rushwa iathiri uchumi wa nchi.” Hii inaonesha kuwa wananchi wengi wapo tayari kwa kiwango fulani kukubali maendeleo yachelewe kama italeta haki na uadilifu zaidi kwenye jamii.

Katika suala la njia bora za kupunguza rushwa, wananchi wanaonekana kugawanyika kwa kiasi kikubwa. Walipoambiwa wachague ni njia ipi nzuri zaidi - kutatua kesi za zamani za rushwa na kuwaadhibu watuhumiwa, au kufanya kubana mianya ya vitendo vya rushwa kufanyika, – asilimia 57 walisema ni muhimu zaidi kushughulikia matendo makubwa ya rushwa kuliko madogo, ukilinganisha na asilimia 43 waliochagua usimamizi wa vitendo vya rushwa.


Vile vile kuna mgawanyiko wa nusu kwa nusu kati ya wale waliosema rushwa ni sehemu ya ubepari isiyoepukika (asilimia 46), na wale waliosema ubepari bila rushwa inawezekana (asilimia 54).

Upo ufafanuzi mdogo kuhusu masuala mawili yenye mvutano kwenye mjadala wa sasa wa siasa. Asilimia 65 ya wananchi wanasema wanaotuhumiwa kwa vitendo vya rushwa wanayo haki ya kujitetea, ukilinganisha na asilimia 35 wanaosema haki ya watuhumiwa iwekwe kando. Vile vile, asilimia 59 ya wananchi wanasema iwapo ushahidi utaonesha rais wa zamani alihusika na rushwa, asipewe kinga/upendeleo wowote.

**Kielelezo cha 9: Nitakusomea makundi mawili ya kauli, tafadhali chagua kauli unayokubaliana nayo zaidi:**



**Kielelezo cha 9: Nitakusomea makundi mawili ya kauli, tafadhali chagua kauli unayokubaliana nayo zaidi:**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 21 (Julai-Agosti 2017)

## Jambo la 5: Idadi kubwa ya wananchi hawajasikia tuhuma kubwa za rushwa, ikiwemo kesi ya Acacia/mchanga wa madini

Idadi kubwa ya wananchi hawafahamu kuhusu kesi za tuhuma za rushwa, hata zile ambazo zimetawala vichwa vya habari mara kwa mara. Asilimia 59 hawajasikia kuhusu kesi ya Acacia/ mchanga wa madini (makinikia) na asilimia 59 hawajasikia kuhusu kashfa ya ukwepaji kodi bandarini. Asilimia 47 ya wananchi wanafahamu kashfa ya Escrow, na asilimia 63 wanafahamu kuhusu kesi ya Richmond, japokuwa matukio haya yalitokea karibu miaka kumi iliyopita.

Uelewa kuhusu kesi hizi ni mdogo kuliko ufahamu wake. Asilimia 12 wanaelewa kwa kina kuhusu kesi ya Acacia/mchanga wa madini, na asilimia 11 wanaelewa kuhusu kesi ya Richmond.

**Kielelezo cha 10: Je, unafahamu kesi ipi kati ya kesi zifuatazo?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 21 (Julai-Agosti 2017)

Wanaume wana uwezekano mkubwa kuliko wanawake kufahamu na kuelewa kuhusu kesi hizi. Kwa mfano, asilimia 75 ya wananume wamesikia kuhusu kashfa ya Richmond, ukilinganisha na asilimia 50 ya wanawake.

Vile vile, wakazi wa maeneo ya mijini wana uwezekano mkubwa zaidi kuliko wenzao wa vijijini kusikia kuhusu Richmond na Acacia/mchanga wa madini.


**Kielelzo cha 11: Ipi kati ya kesi zifuatazo unaifahamu?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*,
Awamu ya 21 (Julai-Agosti 2017)

Miongoni mwa wale wanaozifahamu hizi kesi, asilimia 84 kati yao wamesema serikali inashughulikia vizuri kesi ya Acacia/mchanga wa madini, na asilimia 67 wamesema hivyo hivyo kuhusu serikali kushughulikia kesi ya ukwepaji wa kodi bandarini. Asilimia 25 ya wananchi wamesema serikali ilishughulikia vizuri kesi ya Richmond, na asilimia 38 wamesema hivyo hivyo kuhusu kesi ya Escrow.

**Kielelezo cha 12: Ni kwa kiwango gani unafikiri serikali inashughulikia kila kesi? (miongoni mwa wanaofahamu kesi hizi, % ya wanaojibu "vizuri")**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*,
Awamu ya 21 (Julai-Agosti 2017)

Kuna masuala mawili ya kutafakari yanayojitokeza katika jambo hili. Kwanza; katika kesi ambazo serikali imepongezwa kutokana na namna inavyozishughulikia ni kesi mbili ambazo ziliibuliwa na serikali yenyewe. Katika kesi nyingine ambazo ziliibuliwa na vyombo vya habari, asasi za kiraia na vyama vya upinzani, serikali ilichelewa kukubali kuwa kuna tatizo mpaka pale ushahidi uliposhamiri. Pengine ni muhimu sana kwa Serikali kuziibua na kuzishughulikia kesi kwani ndio kitendo kinachopongezwa zaidi na wananchi.


Hata hivyo, serikali imepata alama za juu kutokana na namna inavyoshughulikia kesi za rushwa za hivi karibuni, na viwango vya chini kwa kesi za zamani. Hivyo basi huenda wananchi wameona kesi za zamani hazijatatuliwa ipasavyo, na pengine viwango vya juu wanavyoipa serikali kwa namna inavyoshughulikia kesi za sasa vitashuka endapo utatuzi unaoridhisha wa kesi hizo hautafikiwa.

## Jambo la 6: Nusu ya wananchi wanasema wanasiasa wanaojihusisha na rushwa wafungwe gerezani

Asilimia 49 ya Watanzania wangependa mwanasiasa mkubwa aadhibiwe kwa kufungwa gerezani iwapo amegundulika kuwa ameiibia serikali shilingi milioni 100. Hukumu kama hiyo inaungwa mkono kwenye kesi nyingine mbili za mfano – askari wa barabarani anayepokea rushwa ya shilingi 20,000 ili asimuandikie afisa wa serikali kosa, na pia askari anayepokea rushwa ya shilingi milioni tano. Kwa kesi ya askari kupokea rushwa ya shilingi 20,000, asilimia 39 ya wananchi walichagua hukumu ya kifungo gerezani.

Asilimia 31 ya wananchi wanasema inatosha kwa mwanasiasa kurudisha fedha alizoiba (shilingi milioni 100), lakini kwa wizi mdogo (eflu 20,000 na milioni 5), kurudisha fedha hizo haionekana kama adhabu inayofaa. Asilimia 10 wanasema (walioiba fedha nyingi) waondolewe kwenye ofisi za umma, ukilinganisha na mfano afisa ardhi (asilimia 18) na askari wa barabarani (asilimia 30) walioiba fedha kidogo.

**Kielelezo cha 13: Unadhani nini kifanyike pale ambapo watu wafuatao wamekutwa na hatia ya kupokea rushwa?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 21 (Julai-Agosti 2017)

## Jambo la 7: Mwananchi mmoja kati ya watatu anafahamu kuhusu mahakama ya rushwa; wawili kati ya watatu wanasema itafanya kazi kwa ufanisi

Asilimia 32 ya wananchi wanafahamu kuhusu kuanzishwa kwa mahakama mpya ya rushwa (ambayo ilianza rasmi utendaji wake Septemba 2016)[4], na wananchi wawili kati ya watatu wanasema itafanya kazi nzuri katika kupambana na rushwa.

**Kielelezo cha 14: Je, unafahamu kuhusu uwepo wa mahakama ya rushwa? Kwa kiwango gani itafanya kazi kwa ufanisi katika kupambana na rushwa nchini Tanzania?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 21 (Julai-Agosti 2017)

Wakati huo huo, mapema mwaka 2017, wananchi walikuwa na mashaka juu ya watu wenye nguvu na mamlaka iwapo wataadhibiwa kwa mujibu wa sheria pindi wanapofanya uhalifu; wananchi wawili kati ya watatu walisema kuwa watumishi wa umma (asilimia 68), maafisa wa polisi (asilimia 69), viongozi waandamizi wa serikali (asilimia 72) na matajiri (asilimia 74) huadhibiwa mara chache au hawaadhibiwi kabisa.[5]

## Jambo la 8: Idadi ya wananchi wanaosema kiwango cha rushwa kimepungua imeongezeka


Asilimia 85 ya wananchi wanasema rushwa imepungua nchini Tanzania. Asilimia 7 wanaona kama rushwa imeongezeka ndani ya miaka mitano iliyopita.

Swali hilo hilo lilipoulizwa mwaka 2014, asilimia 78 walisema rushwa ilikuwa juu ikilinganishwa na miaka 10 iliyopita (2004).

4 http://allafrica.com/stories/201609080140.html

5 *Sauti za Wananchi*, Hapa Usalama tu?, Julai 2017


**Kielelezo cha 15: Je, unalinganishaje kiwango cha rushwa kwa Tanzania ya leo na kiwango cha rushwa kilivyokuwa miaka michache iliyopita?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Kundi la 1 awamu ya 19 (Juni 2014) na Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Kundi la 2 Awamu ya 21 (Julai-Agosti 2017)

Vile vile, wananchi sasa wana uhakika zaidi kuhusu uwezekano wa kupungua kwa rushwa nchini Tanzania. Mwaka 2014, asilimia 51 ya wananchi walisema rushwa haiwezi kupunguzwa kabisa lakini kwa sasa, ni asilimia 10 tu wanasema hivyo. Hata hivyo, pamoja na kuongezeka kwa uhakika huu, asilimia 27 bado inasema kwamba rushwa inaweza kukomeshwa au kupunguzwa kwa kiasi kikubwa nchini Tanzania, huku asilimia 63 wakisema inaweza kupunguzwa kwa kiwango fulani.


**Kielelezo cha 16: Kwa kiwango gani unafikiri rushwa inaweza kupunguzwa nchini Tanzania?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Kundi la 1 awamu ya 19 (Juni 2014) na Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Kundi la 2 Awamu ya 21 (Julai-Agosti 2017)

Walipoulizwa kuhusu kauli ya kiongozi wa zamani wa TAKUKURU kuwa baadhi ya watu nchini Tanzania "hawashikiki," asilimia 46 walisema kauli hiyo kwa sasa "haina ukweli." Asilimia 62 ya wananchi walisema ilikuwa ni "ukweli mtupu" miaka mitano iliyopita, lakini ni asilimia 20 tu inayosema hivyo sasa.

**Kielelezo cha 17: kiongozi aliyepita wa taasisi ya kupambana na rushwa, TAKUKURU, alinukuliwa akisema kuwa kuna baadhi ya viongozi waandamizi nchini Tanzania ambao walikuwa "hawashikiki." Ni kwa kiwango gani kauli hiyo ni sahihi hivi sasa? Na miaka mitano iliyopita?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 21 (Julai-Agosti 2017)

Wananchi hawaoni kama kuchagua upinzani ni njia nzuri ya kupunguza rushwa. Hii inajidhihirisha pale ambapo asilimia 18 ya wananchi wanasema iwapo upinzani ungekuwa madarakani ungefanya kazi nzuri zaidi katika kupambana na rushwa nchini Tanzania, ukilinganisha na asilimia 73 ambao hawakubaliani na kauli hiyo (haijaoneshwa kwenye jedwali).

# 3. Hitimisho

Matokeo ya muhtasari huu kwa kiasi fulani yanaonesha kuwa wananchi wanaidhinisha mikakati ya serikali ya awamu ya tano katika kupambana na rushwa. Wananchi wanasema kwa sasa hawakutani sana na vitendo vya rushwa kutoka taasisi za serikali (na zisizo za serikali) tofauti na ilivyokuwa mwaka 2013, na wanaona kuwa rushwa imepungua kwenye taasisi karibu zote. Aidha, wanasema kiwango cha rushwa nchini Tanzania kwa ujumla ni cha chini ukilinganisha na miaka mitano iliyopita, tukikumbuka kwamba, mwaka 2014 wananchi wengi walisema kiwango cha rushwa kimeongezeka. Wananchi kwa sasa wana matumani makubwa kuhusu uwezekano wa rushwa kupungua kuliko ilivyokuwa mwaka 2014.

Haya ni mafanikio makubwa na yanapaswa kupongezwa. Hata hivyo, yanapaswa kwenda sambamba na tahadhari kadhaa.

Kwanza, inawezekana kukawa na tofauti kubwa kati ya mtazamo wa wananchi kuhusu rushwa (na hata wanavyozungumzia uzoefu wao kuhusu rushwa) na hali halisi. Kwa mantiki nyingine, watu wanaweza kudhani rushwa imepungua hususani pale ambapo mapambano dhidi ya rushwa yamejipatia umaarufu mkubwa na kutawala vyombo vya habari. Ni vigumu sana kupima viwango halisi vya rushwa kwa usahihi, na muhtasari huu haudai sifa hiyo. Zaidi, mitazamo ya wananchi inaweza kuwa inategemea uzoefu wao wa rushwa "ndogo," wakati wa kupata huduma za umma.

Pili, kuna dalili kuwa wananchi hawaungi mkono jinsi serikali inavyopambana na rushwa. Asilimia kubwa wanasema ni muhimu haki za msingi za watuhumiwa zikaheshimiwa, na iwapo marais wa zamani watabainika kujihusisha na rushwa wasipewe kinga. Hata hivyo masuala yote mawili yanaenda kinyume na kauli za viongozi waandamizi wa serikali. Wananchi wamegawanyika nusu kwa nusu kuhusu iwapo suala la rushwa linashughulikiwa vizuri kwa kutatua kesi za zamani na

kuwawajibisha wahusika au kwa kuweka mfumo ambao utafanya iwe vigumu kwa watu kufanya makosa hayo. Wakati serikali ikiwa imejikita kuwashughulikia wala rushwa, inasemekana imerudi nyuma katika kuweka mikakati ya kuhakikisha watu hawafanyi vitendo vya rushwa, kwa mfano, kwa kubana uhuru wa vyombo vya habari na kukataza shughuli za wanasiasa wa upinzani. Hivi karibuni ilibainika kuwa wananchi wengi bado wanaamini kuwa watu wenye nguvu nchini Tanzania wapo juu ya sheria.[6]

Tatu, uelewa wa wananchi kuhusu kesi kubwa za tuhuma za rushwa nao ni muhimu. Idadi kubwa ya wananchi hawafahamu kesi hizo, zikiwemo zile ambazo zilitawala vichwa vya habari ndani ya miezi michache iliyopita (kama vile kesi ya Acacia/mchanga wa madini) na zile za miaka 3-4 iliyopita (kama vile kesi ya Escrow). Pale ambapo uelewa wa wananchi ni mdogo, hakuna uwezekano wa wao kupima kwa usahihi, kwa mfano, kama bado wapo wale wanaoitwa "hawakamatiki" au kama kweli rushwa imepungua.

Hata hivyo, mtazamo kuwa rushwa imepungua ni wa muhimu. Pale ambapo wananchi wanafikiri kuwa kuna mabadiliko yanatokea, na wanakuwa na uhakika kuwa upo uwezekano wa rushwa kupungua, inaweza kusaidia kujenga imani na serikali na kuonesha wengine kuwa uadilifu ni kitu cha thamani. Hii pia inaweza kuwapa wananchi ujasiri zaidi wa kutoa taarifa za rushwa. Imani na mitazamo hiyo inaweza kuleta matokeo chanya kwenye tabia na kubadilisha maadili ya jamii.

Hata hivyo, changamoto kubwa inayojitokeza kutoka kwenye muhtasari ni kuhusu wakosoaji wa serikali, hususani wale ambao wamekuwa wakijaribu kwa miaka mingi kuishawishi serikali kulipa uzito suala la rushwa na ambao sasa wamejikuta wakiikosoa serikali ambayo inafanya hivyo hivi sasa, kwa kusema kuwa inafanya "katika njia isiyo sahihi." Kwa kundi hili, viwango vidogo vya uelewa kuhusu kesi za zamani unatia mashaka makubwa. Baadhi yao, kasi yao ya kisiasa ilijengwa kwa kiasi kikubwa katika kuzifanya kesi hizo zifahamike kwa wananchi. Vile vile, miongoni mwa wananchi wanaofahamu kesi hizo ambazo zilizotokea tangu uchaguzi wa mwaka 2015, wengi wao wanaafiki namna serikali inavyozishughulikia. Na idadi kubwa ya wananchi hawadhani kuwa upinzani ungeshughulikia suala la rushwa vizuri kuliko uongozi wa sasa unavyofanya. Kwa kifupi, hapo baadae huenda wapinzani wakapata nafasi ndogo ya kuungwa mkono na wananchi kupitia agenda ya mapambano dhidi ya rushwa.

Pamoja na hilo, tusiangukie kwenye mtego wa kuhitimisha kwamba, kuwa wakali na kutofuata utaratibu wa kuwashtaki wale wanaotuhumiwa kwa rushwa kuwa kumepunguza rushwa. Hakuna ushahidi hapa unaounga mkono mtazamo huu. Hata hivyo, kuna sababu nyingi nzuri za kulinda na kuimarisha uzingatiaji wa utaratibu wakati wa kupambana na rushwa, kama vile, kuhakikisha kuwa wenye hatia tu ndiyo wanaadhibiwa, kufuta tuhuma za uongo, na kujenga imani miongoni mwa watumishi wa umma. Kupambana na rushwa kwa kumtafuta mchawi, na hukumu za kujionesha, ni dalili za serikali ya mabavu, ni kama mtazamo ule usio na mantiki usemao kuwa matokeo huhalalisha mbinu iliyotumika. Mitazamo na mijadala hiyo huvutia wananchi wengi ili kuficha ukosefu wa ushahidi na uhakika pia.

Hakuna sababu yoyote inayozuia serikali kuwa kali katika mapambano dhidi ya rushwa na wakati huo huo inawataka wafuate utaratibu unaopaswa. Na wakati tukiwa kwenye mapambano haya, hamna sababu ya kuzuia mijadala na ukosoaji.

---

6 Safety first? Security, policing and justice in Tanzania – *Sauti za Wananchi brief, July 2017*